

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA SABA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA NANE

5 MEI, 2017

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA NANE TAREHE 5 MEI, 2017

I. DUA:

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi. Mwenyekiti wa Bunge (Mhe. Mussa Azzan Zungu, alisoma Dua.

Makatibu mezani:

1. Ndugu Theonest Ruhilabake
2. Ndugu Charles Mloka

II. HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo aliwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mhe. Juma Nkamia aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

III. MASWALI

OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa na Serikali.

Swali Na. 145: Mhe. Faida Mohammed Bakari

Nyongeza: Mhe. Faida M. Bakari
Mhe. Andrew J. Chenge

Mhe. Ally Mohamed Keissy
Mhe. Ester M. Mmasi
Mhe. Cecilia D. Paresso
Mhe. Masoud A. Salim
Mhe. Munde A. Tambwe

Mwenyekiti aliruhusu Maswali ya Nyongeza kwa idadi hiyo ya Wabunge chini ya Kanuni ya 5 na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) Mhe. George B. Simbachawene alijibu idadi hiyo iliruhusiwa kutokana na unyeti wa swali hili kuwagusa Wabunge wengi.

Swali Na. 146: Mhe. Ezekiel Maige aliuliza Sali kwa niaba ya Mhe. Ahmed Ally Salum

Nyongeza: Mhe. Ezekiel Maige

Swali Na. 147: Mhe. Mwantumu Dau Haji

Nyongeza: Mhe. Mwantumu Dau Haji

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

Swali Na. 148: Mhe. Pascal Yohana Haonga

Nyongeza: Mhe. Pascal Yohana Haonga

Swali Na. 149: Mhe. Dkt. Mary M. Nagu

Nyongeza: Mhe. Dkt. Mary M. Nagu

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Swali Na. 150: Mhe. Halima Ali Mohammed

Nyongeza: Mhe. Halima Ali Mohammed

Swali Na. 151: Mhe. Daudi Iddi Mpakate

Nyongeza: Mhe. Daudi Iddi Mpakate

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Swali Na. 152: Mhe. Japhet Nailonga Hasunga

Nyongeza: Mhe. Japhet Nailonga Hasunga

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Swali Na. 153: Mhe. Zainab Mussa Bakari

Nyongeza: Mhe. Zainab Mussa Bakari

WIZARA YA NISHATI NA MADINI

Swali Na. 154: Mhe. Zitto Z. Kabwe

Nyongeza: Mhe. Zitto Z. Kabwe

IV. MATANGAZO:

1. Wageni wa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Mhe. Dkt. Harisson Mwakyembe)

- Ndugu Elisante Ole Gabriel – Katibu Mkuu
- Ndugu Nuru Millao – Naibu Katibu Mkuu
- Ndugu Dkt. Hassa Abbas – Mkurugenzi wa Habari – Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali
- Ndugu Dkt. Ayoub Rioba – Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji (TBC).

Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maofisa mbalimbali kutoka katika Wizara.

Wasanii, wadau wa sanaa, Wakuu Wanahabari, Utamaduni na Wadau wa Michezo.

2. Wageni wa Waheshiwa Wabunge na Wanafunzi waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni.
3. Mashindano ya mpira wa miguu, mpira wa pete na mpira wa kikapu kati ya NMB na Bunge tarehe 6 Mei, 2017. Mgeni Rasmi atakuwa Mhe. Spika.

V. MWONGOZO WA SPIKA

1. Mhe. Pauline Gekul aliomba mwongozo chini ya Kanuni 68(7) kuhusu swali la Mhe. Faida Bakari Na. 145 kuhusu Mfuko wa Jimbo, aliomba Kiti kitoe maelekezo kwa Serikali kufafanua kwa nini Serikali imepunguza fedha za Mfuko wa Jimbo bila Wabunge kujua.

Mwenyekiti alijibu kuwa Swali la msingi lilihusu usawa kwa Wabunge katika matumizi ya Mfuko wa Jimbo. Hivyo, alielekeza kuwa hakuna mwongozo.

2. Mhe. Mchengelwa aliomba mwongozo chini ya Kanuni 68(7) na kukiomba Kiti kimpe mwongozo kwa mamlaka yaliyofafanuliwa chini ya Kanuni 5, akirejea matumizi ya Kanuni 103(1) – (4) wakati wa kushika mshahara wa Waziri katika Hotuba iliyopita wakati alipotumia fursa ya kuomba ufanuzi katika Kamati ya Matumizi kuwa hakuwahi kujibiwa ipasavyo.

Mwenyekiti alisema na kufafanua kuwa Kanuni inayohusu ufanuzi na hasa kutoa shilingi inahusu jambo la kisera na kwamba suala alilodai halikutolewa ufanuzi wa kutosha halikuwa la kisera. Hata hivyo, alielekeza aonane na Waziri anayehusika kupata maelezo ya ziada.

VI. UFAFANUZI WA MWENYEKITI KUHUDU HAKI, KINGA NA MADARAKA YA BUNGE

Mwenyekiti alitoa ufanuzi kwa muhtasari kuhusu matumizi sahihi ya Haki za Bunge akirejea Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Ibara ya 89 na mwongozo uliotolewa kwa maandishi maarufu wa masuala ya Bunge, Erakine May, kuhusu haki hizo kuwa zinasimamiwa na Spika/Kiti kila Kikao kinapoanza. Aidha, alisisitiza kuwa pamoja na Wabunge kudai kuwa haki hizo zimefafanuliwa katika Ibara ya 100 na haki hizo zimebekewa mpaka katika Ibara ya 89 inayotoa fursa kwa Bunge kutunga Kanuni zake. Moja ya mipaka hiyo ni kutozungumzia masuala yaliyopo Mahakamani.

Baada ya kutoa ufanuzi huo alisema alipitia Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na Hotuba ya Wizara kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Kwa mujibu wa masharti ya Kanuni 64(1) (e), alisema amegundua kuwa hotuba ya Kambi ya Upinzani imerudia maneno ya kuudhi yaliyotolewa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wakati wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo Kiti kilikwishaamua yaondolewe. Hivyo, kwa mamlaka yake alielekeza kuwa maneno ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani yaliyomo uk. 6 – 10, uk 35 – 45 yaondolewe na kuonya kuwa Taarifa nyingine zitakazokiuka masharti ya Kanuni ya Kamati au Wizara atazichukulia hatua.

Mwisho, Kiti kilitoa fursa kwa Mbunge yeote asiyeridhika na maamuzi ya Kiti kukata Rufaa chini ya Kanuni ya 5(4).

VII. HOJA ZA SERIKALI

Baada ya ufanuzi Mwenyekiti alimwita Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuwasilisha Hoja yake.

Mhe. Juma Nkamia aliwasilisha maoni ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Joseph O. Mbilinyi aliwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

MWONGOZO WA SPIKA

Mhe. Tundu Lissu aliomba mwongozo kuhusu Serikali kuamulia Kambi ya Upinzani nini cha kusema kabla hata haijasoma jambo linaloua Bunge.

Mhe. Jenista Mhagama – Serikali hakiamulii kitinini cha kufanya bali kuhakikisha taratibu/kanuni zinafuatwa

Mhe. Ester Bulaya aliomba mwongozo kwamba Serikali inawaamulia Kambi ya Upinzani nini cha kufanya.

Kiti kilitoa mwongozo kwamba hakiongozwi na Serikali bali ni kwa Kanuni na Kifungu 8 Kiti hakipaswi kuwa na mlengo wa Siasa. Kwa vile alishatoa mwongozo kuhusu jambo hili la hotuba hii ya upinzani kutosomwa baadhi ya maneno na kwamba yejote asiyeridhika atumie Kanuni 5 kukata rufaa.

Baada ya mwongozo huo Mhe. Joseph Mbilinyi alitakiwa kuendelea bila kusoma yaliyotolea jambo ambalo hakufanya na hivyo kuamriwa kukaa kwa kukiuka maelekezo.

Majadiliano ya jumla yalifuata na wafuatao walichangia:-

- | | | |
|--------------------------------|---|-----|
| 1. Mhe. Juma Selemani Nkamia | - | CCM |
| 2. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda | - | CCM |

Taarifa

Mhe. Tundu A. Lissu alimpa taarifa mzungumzaji kwamba Mwenge wa Uhuru siyo nembo ya Taifa kwa vile haimo katika Sheria ya Nembo za Taifa lakini mzungumzaji alikataa taarifa hiyo na aliendelea kuchangia.

- | | | |
|--------------------------------|---|---------|
| 3. Mhe. Cosato David Chumi | - | CCM |
| 4. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi | - | CHADEMA |
| 5. Mhe. Tundu Antiphas Lissu | - | CHADEMA |

VIII. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 7:00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11:00 jioni.

IX. BUNGE KUREJEA

Saa 11:00 jioni Bunge lilirejea na Wabunge wafuatao waliendelea kuchangia Hoja baada ya kuitwa na Mwenyekiti.

6. Mhe. Venance Methusalah Mwamoto	-	CCM
7. Mhe. Amina Saleh Mollel	-	CCM
8. Mhe. Martha Moses Mlata	-	CCM
9. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi	-	CCM
10. Mhe. Salum Mwinyi Rehani	-	CCM
11. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo	-	CCM
12. Mhe. Ali Saleh Ali	-	CUF
13. Mhe. Ahmed Juma Ngwali	-	CUF
14. Mhe. Joseph George Kakunda	-	CCM
15. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa	-	CCM
16. Mhe. Kiteto Zawadi Konshuma	-	CCM
17. Godbless Jonathan Lema	-	CHADEMA

Kuhusu Utaratibu

Mhe. George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEM) alisimama kuhusu utaratibu chini ya Kanuni ya 64(2) na 72(2) akitaka Mhe. Lema afute kauli yake kuhusu kufichwa kwa Katibu Mkuu wa CCM, Abdulrahman Kinana kama alivyonukuu katika mitandao ya jamii. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mhe. Jenista Joakim Mhagama alikanusha taarifa hizo akidai si za kweli na kwamba Mhe. Kinana yupo na alikitaka Kiti kimtake Mhe. Lema afute maneno yake.

Mweyekiti alitoa maelekezo kuwa Mhe. Lema afute maneno yake ili kuondolea hofu familia yake na jamii kuhusu habari ambazo hana uhakika nazo.

Mhe. Lema alifuta kauli kwa kueleza matumaini yake kuwa amehakikshiwa na Waziri wa Nchi kuwa Mhe. Kinana ambaye ni mpiga kura wake yupo na hajafichwa.

- | | | | |
|-----|----------------------------|---|---------|
| 18. | Mhe. Devota Mathew Minja | - | CHADEMA |
| 19. | Mhe. Omar Mohamed Kigua | - | CCM |
| 20. | Mhe. Richard Phili Mbogo | - | CCM |
| 21. | Mhe. Richard Mganga Ndassa | - | CCM |

X. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 1:37 usiku Bunge lilahirishwa hadi Jumatatu tarehe 8 Mei, 2017 saa 3:00 asubuhi.